# Muhtasari Wa Misingi Iliyojengewa Ushia Al-Imaamiya Al-Ithnaasheria

"Haiwezekani kuwasogeza Mashia wawe karibu na misingi ya madhehebu mengine yote ya Kislamu"

Na Muhibbu Al-Dini Al-Khatwiibi

# Muhtasari Wa Misingi Iliyojengewa Ushia Al-Imaamiya Al-Ithnaasheria

*“Haiwezekani kuwasogeza Mashia wawe karibu na misingi ya madhehebu mengine yote ya Kislamu”*

Na Muhibbu Al-Dini Al-Khatwiibi

**Yaliyomo**


- Utangulizi
- Muhtasari
- Fiqihi ya Kiislamu
- Namna Mashia wanavyoongopa hadi kumwongopea Imamu Ali, Allah amuwie radhi
- Rai ya Mashia kwa viongozi wa Kiislamu wa Kisunni
- Kumtukuza aliyemuua Omari, Allah amuwie radhi
- Itikadi (Akida) ya kurejea duniani, kwa Imamu Al-Mahdi
- Kujificha kwa maimamu wa Kishia
- Kuwa pamoja na Waislamu wengine

## Utangulizi

Sifa njema anastahiki Allah Mola wa viumbe vyote. Na, Rehema na amani ziwe juu ya Mtume Muhammad, mbora wa Mitume yote, pia ziwe juu ya aali zake na maswahaba zake wote.

Ama baadu: "Kwa hakika wito wa kuwaweka karibu Masshia Al-Imaamiya Al-Ithnaasheria na Masunni, Al-Zaidiya au Al-Ibaadhiya ulioitishwa katika miaka ya hivi karibuni, umenifanya niichunguze kisomi mada hii".

Mwandishi wa Kiislamu, Al-Sayid Muhibbudini Al-Khatwiibu amefanya utafiti huu katika vitabu tegemezi vya Kishia kwa lengo la kupata njia za kujongeleana. Ikambainikia kuwa; haiwezekani kuwepo jambo hilo, kwa kuwa waanzilishi wa misingi ya dini ya Kishia hawakutoa nafasi ya kuwepo kujongeleana katika misingi ya dini yao, kwani waliianzisha dini yao juu ya nguzo zinazopingana na yale aliyokuja nayo Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake. Pia yanapingana na yale aliyowalingania Maswahaba zake, kisha akawaacha wakiwa katika njia ya wazi inayoangaza kiasi cha kwamba hakuna atakayeiacha njia hiyo bila ya kuangamia.

Kwa kuwa nukuu zilizomo katika utafiti huu zimenukuliwa kutoka katika vitabu vya kutegemewa na kundi la Al-Imaamiya Al-Ithnaasheria. Ushahidi wa nambari za kurasa umetolewa. Pia chapa za vitabu vilivyotumika zimebainishwa. Hadi hapo, mtu yoyote hatoweza kupinga vitu hivyo. Kwa hiyo tumeonelea tuuweke utafiti huu machoni mwa watu ili 'Awe hai atakayekuwa hai kwa ushahidi na aangamie atakayeangamia kwa ushahidi' na Allah ni mlinzi wa walioongoka.

Umeandikwa na

Muhammad Naswiifu.

**Muhtasari**

Kujongeleana baina ya Waislamu kwa fikra, mambo wanayoyakubali, mielekeo, mitazamo na malengo yao ni miongoni mwa malengo makuu ya Uislamu. Na hiyo ndio njia kuu ya kuupa nguvu, mwamko na kuutengeneza Uislamu. Na jambo hilo ni jambo la heri kwa umma wao na umoja wao katika kila zama na kila sehemu.

Wito wa kujongeleana kama utakuwa hauna lengo baya, wala hautaleta madhara katika ufafanuzi wake, madhara yanayozidi manufaa yake, basi itamlazimu kila Muislamu auitikie na asaidiane na Waislamu wengine kuufanikisha.

Katika miaka ya hivi karibuni habari za wito huu zimekuwa nyingi, kisha athari zake zikaendelea hadi zikafika Chuo Kikuu cha Al-Azhar. Na kwa kuwa Al-Azhar ni chuo kikuu mashuhuri kabisa cha dini kwa upande wa Masunni wanaonasibiana na madhehebu manne ya kifiqihi ya Kisunni. Al-Azhar ikalichukua wazo hilo la kujongeleana kwa mapana zaidi kuliko upeo wa mipaka yake tena bila kusita, tangu zama za Swalaahudini Al-Ayuubi hadi leo. Al-Azhar ikatoka katika wigo huo na kuelekea kutaka kuyajua madhehebu mengine.

Dhehebu la mwanzo ni Al-Shia Al-Imaamiya Al-Ithnaasheria. Hadi mida hii, Al-Azhar bado ipo mwanzoni mwa njia hii. Kwa hiyo mada hii ya hatari inafaa kuifanyia uchunguzi, utafiti na kuionesha kwa kila Muislamu mwenye ujuzi na jambo hili, ili ajue mambo yanayofungamana na mada hii, na yale yanayopelekea kuijua miongoni mwa vitu vinavyooneka na vinavyotokea.

Kwa kuwa kawaida ya mambo ya dini yana hisia kali, kwa hiyo inatakiwa kuwe na hekima, ujuzi na usahihi katika kuyashughulikia. Na mwenye kuyatafiti anapaswa awe na ufahamu wa kujua vitu vinavyojiingiza, pia awe na nuru kutoka kwa Allah pamoja na uadilifu katika kuchambua na kuhukumu, ili kazi yake ilete matokeo yanayotakiwa. Na, inshaallah, hayo matokeo yalete manufaa kwa umma wa Kiislamu.

Katika jambo hili, pia katika kila jambo lenye mafungamano ya zaidi ya pande moja, kitu cha kwanza tunachokiona, ni kwamba; sababu kubwa ya kufanikiwa ni kuwepo kusikilizana baina ya pande mbili au baina ya pande zinazofungamana. Kwa mfano swala la kuwajongelesha Masunni na Mashia: Kilichoonekana ni kuwa, Misri kumeanzishwa jengo maalum kwa ajili ya wito wa kuzijongelesha pande mbili hizo.

Jengo hilo linagharamiwa na bajeti rasmi ya dola la Kishia. Na hilo dola karimu la Kishia limetupatia sisi Massuni kipaumbele kwa ukarimu huu na kutufanya tuwe watu wa kipekee tunaopokea mali hizi rasmi. Na dola hiyo hiyo ikajibana yeye yenyewe haikujiwekea wala kuwawekea watu wa dhehebu lake jengo kama hilo. Wala haikutoa mali kama hizi ilizozitoa ili kuanzisha jengo la kujongeleana huko Tehran au Qum au Najafu au Jabalu Aamilu au sehemu nyingine yoyote miongoni mwa vyuo vya kulingania na kusambaza dhehebu la Kishia.[1]

Kwa hakika vituo vya kusambaza wito huu wa Kishia vimeanzishwa katika miaka ya hivi karibuni, lakini cha ajabu wito huo unasigana na vitabu vinavyovunja wazo la kufahamiana na kujongeleana kwa kiasi cha kuifanya miili yetu inyanyapae. Miongoni mwa vitabu hivyo ni kitabu kiitwacho "Al-Zahraau" kitabu hiki kina juzuu tatu, kimesambazwa na wanazuoni wa Najafu waliosema ndani ya kitabu hicho kuwa amiri Al-Muuminina Omari bin Al-Khatwaabi alikuwa na ugojnwa usiopona ila kwa maji ya wanamume! Ustadhi Al-Bashiri Al-Ibrahimiyu, shehe wa wanazuoni wa Algeria ameliona jambo hilo alipotembelea Iraq kwa mara ya kwanza.

Pepo mchafu anayetoa uovu wa kimadhehebu kama huu, ndiye anayepaswa awe na shida zaidi ya wito wa kujongeleana kuliko sisi Ahlisunna tunavyohitaji jambo kama hili. Ikiwa tofauti ya msingi baina yetu na wao imejengeka katika madai yao kuwa wao wanawapenda zaidi Ahli-beiti. Pia katika dai lao la kuwa wao wanaficha – bali wanadhihirisha – chuki na mfundo dhidi ya Maswahaba wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake. Maswahaba ambao, wameusaidia Uislamu usimame mabegani mwao.

Roho chafu hizo zimefikia upeo wa kusema maneno machafu kama haya kwa amiri Al-Muuminina Omari bin Al-Khatwaabi, Allah amuwie radhi. Uadilifu unawataka wao waanze kupunguza chuki na mifundo yao dhidi ya Maimamu wa mwanzo wa Kiislamu. Pia wawashukuru Ahlisunna kwa kuwa na msimamo mzuri kwa Aali baiti, wala hawawatii dosari Aali baiti kwa chochote miongoni mwa mambo ya wajibu katika kuwatukuza na kuwakarimu, ispokuwa kama mapungufu yetu kwa upande wa Aali baiti, yatukuwa kwamba sisi hatuwaabudu wao pamoja na Allah, kama

[1]Huku kutoa kipaumbele kumerejewa rejewa sana na watu hao katika zama mbalimbali. Walinganiaji wanaowatuma kwa malengo kama haya ndio wameifanya Iraq ibadilike kutoka katika hali ya kuwa nchi ya Kisunni ikiwa na Mashia wachache na kuwa nchi ya Kishia ikiwa na Masunni wachache. Katika zama za Jalaludini Al-Suyuutwi, mlinganiaji mmoja miongoni mwa walinganiaji wao alifika Misri akitokea Iran. Al-Suyuutwi amemwashiria katika (Al-Haawii Lilfataawii) chapa ya Al-Muniriyat juzuu 1 uk 330. Na kwa sababu ya mlinganiaji huyo wa Kiiran, Al-Suyuutwi alitunga waraka alioupa jina la (Miftaahu Al-Jannat fii Al-Itiswaami Bil-sunnat - yaani funguo za Pepo zipo katika kushikamana na Sunna).

inavyoshuhudiwa katika matendo yanayotekelezwa na upande wa pili unaotaka kuwepo kukurubiana baina yetu na wao, kwa hilo ni sawa.

Kukubaliana lazima kuwe kwa kuafikiana baina ya pande mbili zinazotaka kukurubiana. Wala hakuna kukubaliana bila kukutana chanya na hasi. Harakati za kulingania kuwepo kwa jambo hilo zisiwepo katika upande mmoja tu bila upande wa pili, kama ilivyo sasa hivi.

Kile kinachosemekana kuwa kuna mpango wa kukurubiana wa pande moja wenye jengo moja katika mji mkuu mmoja wa nchi za Ahlisunna nayo ni Misri bila kuwepo katika mji wowote miongoni mwa miji mikuu ya dhehebu la Kishia. Pia vituo vya kusambaza wito huo vimechangamka sana, vikiulingania wito huo na kuvipakazia vituo pinzani.

Vilevile mambo hayo hayo yanasemwa katika suala la kuingiza somo la kukurubiana katika mitaala ya vyuo vya Al-Azhar bila ya kuwa na mkabala unaofanana na hivyo katika vyuo vya kufundisha Ushia. Ama jambo hilo kama litaishia katika hali halisi tuliyonayo sasa hivi – kwa upande mmoja tu – bila kuwa katika pande zote zenye mafungamano nayo. Kwa hakika jambo hilo halitarajiwi kufaulu, na kwa upande mwingine jambo hilo litaleta matokeo yasiyo mazuri kwa upande wa pili. Kwani miongoni mwa njia za kipuuzi zaidi katika kutambulishana ni kuanza katika matawi kabla ya mashina!

## Fiqihi ya Kiislamu

Fiqihi kwa Ahlusunna na fiqihi kwa Mashia hazina msingi mmoja unaokubalika na pande mbili hizi. Sheria za kifiqihi kwa maimamu wane wa Ahlusunna imejengwa juu ya misingi iliyokinyume na misingi iliyojengewa sheria za kifiqihi kwa Mashia. Na endapo kama hakutakuwa na kufahamiana katika misingi na mizizi kabla ya kujishughulisha na matawi.

Pia kama hakutokuwa na makubaliano ya jambo hili kwa pande zote mbili katika vyuo vya kielimu vya kila upande, basi hakuna faida ya kupoteza wakati katika matawi kabla kuishughulikia mizizi. Wala hatumaanishi misingi ya kifiqihi (usulu al-fiqihi), bali tunamaanisha misingi ya dini kwa pande zote mbili kuanzia mizizi yake ya mwanzo.

## Suala la taqiya

Kizuizi cha kwanza kabisa kinachozuia makubaliano ya kweli yenye nia safi baina yetu na wao ni kile kitu wanachokiita “taqiya”. Hiyo ni itikadi ya kidini inayowahalalishia Mashia kujionesha mbele yetu kinyume na

vile wanavyovificha. Kwa hiyo mwenye moyo uliosalimika miongoni mwetu anahadaika na vile wanavyojidhihirisha kwake kwa namna ya mapenzi yao ya kutaka kufahamiana na kukurubiana wakati wao hawataki jambo hilo wala hawalishughulikii jambo hilo, ispokuwa wanataka upande mmoja uwe unahangaikia jambo hilo na upande mwingie ujitenga hautikisi hata unywele mmoja.

Kama mwakilishi wa wazo la taqiya miongoni mwao atafanikiwa kutukinaisha kwamba wao wamepiga hatua fulani kutuelekea. Kwa hakika wafuasi wote wa Kishia, wale maalum na wakawaida watatengana na mwakilishi wa masihara haya. Wala hawatakubaliana na wale wanaowasemea kwa jina lao, kwani watu hao hawana haki ya kuwasemea.

**Kuikosoa Quran Takatifu**

Umefika upeo kuwa, hadi Quran ambayo ilipaswa kuwa rejeo linalotuunganisha sisi na wao kuelekea katika kuukaribia umoja, nayo inakosolewa. Kwa kuwa misingi ya dini kwa upande wao imesimama kutokana na mizizi ya kuzitaawili (kizifasili kwa matashi yao) aya za Quran, na kuzipindua maana zake ziwe kinyume na vile walivyozifahamu Maswahaba kutoka kwa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, au ziwe kinyume na walivyozifahamu maimamu wa Kiislamu kutoka katika kizazi cha walioshushiwa Quran.

Mmoja wa wanazuoni wa Najafu, naye ni Alhaji Miirzara Husein bin Muhammad Taqiyu Al-Nuuriyu Al-Twabrisiyu – aliyefikia upeo wa kutukuzwa na Mashia hadi kufikia kwamba, wakati alipofariki mnamo mwaka 1320 Hijiria, Mashia walimzika katika jengo la Al-Mashhad Al-Murtadhiyyu huko Najafu katika eneo la chumba cha Baanu Al-udhumaa binti Al-Sultani Al-Naasirilidinillahi.

Hilo ni eneo la chumba cha mbele upande wa kuume ndani ya uwanja wa Al-Murtadhiyyu kutokea uapnde wa kibla huko Najafu katika eneo takatifu zaidi kwa Mashia – mwanazuoni huyu wa Najafu, mnamo mwaka 1292 Hijiria akiwa Najafu kwenye kaburi linalonasibishwa na imamu Ali, alitunga kitabu alichokiita kwa jina la: “Faslu Al-Khitwaabi fii Ithibaati Tahriifu Kitaabi Rabbi Al-Arbaabi” yaani uchambuzi wa hotuba katika kuthibitisha kupotoshwa kwa kitabu cha Mola wa miungu.

Katika kitabu hicho amekusanya mamia ya maandiko kutoka kwa wanazuoni wa Kishia na mujitahidi wao katika zama mbalimbali. Maandiko yanayosema kuwa Quran imezidishwa na kupunguzwa. Hiki kitabu cha Al-Twabrisiyu kimechapishwa huko Iran mwaka 1298 Hijiria.

Kilipochapishwa kulizuka zogo kwa sababu Mashia walikuwa wanataka kule kutilia mashaka kwao usahihi wa Quran kuwe kumefungika/kumejificha kwa wataalamu wao tu, na badala yake, vitawanywe mamia ya vitabu vinavyokubalika kwao tu.

Kwa hiyo jambo hili (la kuikosoa Quran) lisikusanywe katika kitabu kimoja kitakachochapwa kwa maelfu ya nakala, ili kisije kikaonekana na maadui zao, na kuwe hoja dhidi yao ikitolewa mfano mbele ya macho ya watu wote. Mtazamo huu ulipotolewa na watu wenye akili miongoni mwao, mtunzi wa kitabu hiki aliwapinga na kutunga kitabu kingine alichokiita “Raddu Baadhi Al-Shubuhaati a`n Faslu Al-Khitwaabi fii Ithibaati Tahriifu Kitaabi Rabbi Al-Arbaabi” yaani “Jibu la baadhi ya mazonge kuhusiana kitabu uchambuzi wa hotuba katika kuthibitisha kupotoshwa kwa kitabu cha Mola wa miungu”.

Aliandika utetezi huu mwishoni mwa uhai wake kabla ya kifo chake kwa miaka miwili hivi. Akalipwa kwa juhudi zake hizi za kuthibitisha kuwa Quran imepotoshwa, walimlipa kwa kumzika katika eneo hilo lililobora zaidi katika jengo la Al-Mashhadu Al-Uluwiyu huko Najafu.

Miongoni mwa ushahidi alioutoa mwanazuoni huyu wa Najafu ili athibitishe kuwepo kwa upungufu kwenye Quran; ni katika ukurasa wa 180 wa kitabu chake hicho, pale alipoeleza kuwa kuna sura ambayo Mashia wanaiita (Surat Al-Wilaayati). Ndani ya sura hiyo kumetajwa uwalii wa Ali kama hivi: "Enye mliowaamini Mtume na Walii tuliowapeleka ili wakuongozeni katika njia iliyonyooka… hadi mwisho wake".

Mtu wa kuaminika, mwenye kuaminiwa aitwaye Ustadhi Muhammad Ali Suudiyu – aliyekuwa mkuu wa wataalamu wa wizara ya sheria nchini Misri aliuona Msahafu wa Kiirani ulioandikwa kama mswada ukiwa kwa mustashiriki (mtu asiye Muislamu anayesomea Uislamu) Brayan. Kwa hiyo, Ustadhi Ali Suudiyu aliinakili sura hiyo kwa telegrafu. Na juu ya mistari ya Kiarabu ya sura hiyo kuna tafsiri kwa lugha ya Kiirani.

Na kama Al-Twabrisiyu alivyothibitisha katika kitabu chake (Faslu Al-Khitwaabi fii Ithibaati Tahriifu Kitaabi Rabbi Al-Arbaabi). Pia, kwa hakika jambo hili limethibiti katika kitabu chao (Dibustaani Madhaahibu) kwa lugha ya Kiirani kilichotungwa na Muhsini Faanii Al-Kashimiriyu.

Hiki kitabu kimechapwa huko Iran kwa chapa nyingi. Sura hii iliyosingiziwa kuwa ni ya Allah ilinukuliwa na mustashriki Nuuldikah na kuwekwa katika kitabu chake (Historia ya Misahafu) juzuu ya 2 ukurasa

wa 102 na ikachapishwa na gazeti la Asia kwa Kifaransa (Al-Aasiyawiyatu Al-Faransiyatu) mwaka 1842 ukurusa wa 431 – 4.

Mwanazuoni huyo wa Najafu kama alivyotolea ushahidi aya za sura hiyo kuwa Quran imepotoshwa, vilevile alitolea ushahidi habari iliyopo katika ukurasa wa 289 katika kitabu (Al-Kaafii) chapa ya mwaka 1278 ya huko Iran. Na kitabu hiki kwa Mashia ni sawa na Swahiihi Bukhaari kwa Masunni. Kutoka katika ukurasa huo wa kitabu hicho, yamekujaa maandiko yafuatayo:

“Watu wetu wengi wamepokea kutoka kwa Sahli bin Ziyaad, kutoka kwa Muhammad bin Suleiman, kutoka kwa baadhi ya watu wake kutoka kwa baba Hassan amani iwe juu yake (yaani baba Hassan wa pili naye ni Ali bin Musa Al-Ridhwaa aliyekufa mwaka 206) amesema: "Nilimwambia niwe fidia yako. Kwa hakika sisi tunazisikia aya kwenye Quran sio kama tunazozisikia. Wala hatuwezi kuzisoma vizuri kama zilivyotufikia kutoka kwenu je, tunapata dhambi? Akasema: Hapana, zisomeni kama mlivyojifunza na atakujieni Yule atakayekufunzeni!!

Hapana shaka kuwa maneno haya yametungwa na Mashia na kumsingizia imamu wao Ali bin Musa Al-Ridhwaa, lakini maana ya maneno haya kwa Mashia ni fatuwa kwamba mtu anayesoma Quran kama wanavyojifunza watu wengine katika msahafu wa Athumani hana dhambi. Kisha watu maalum miongoni mwa Mashia watawafundisha Mashia wengine mambo yanayotofautiana na hivyo miongoni mwa vile vitu wanavyodai kuwa vipo au vilikuwepo kwa maimamu zao wa Ahlubeiti.

Kwa kulinganisha baina ya maneno haya yanayodaiwa, na ambayo wanayafanya ni ya siri yao, wao kwa wao wala hawayadhihirishi, kwa kuifanyiakazi itikadi ya taqiya[2] ukiyalinganisha na Quran inayojulikana, iliyosambaa, iliyoandikwa katika Msahafu wa Athumani nayo ndio Quran ambayo bwana Husein bin Muhammad Taqiyu Al-Nuuriyu Al-Twubrisiyu aliitungia kitabu (Faslu Al-Khitwaabi fii Ithibaati Tahriifu Kitaabi Rabbi Al-Arbaabi) ili kuikosoa Quran hii.

Kwa hiyo, Mashia kwa vyovyote vile watakavyojionesha kuwa wametakasika na dhambi ya kitabu cha Al-Nuuriyu Al-Twubrisiyu, watakuwa wanaifanyiakazi itikadi ya taqiya. Kwa hakika kitabu hiki kina mamia ya maandiko kutoka katika vitabu vinavyokubalika vya

[2] Miongoni mwa vitu vilivyoenea kwa Mashia ni jina la 'Taqiyu' na miongoni mwa wenye jina hilo ni baba wa Al-Nuuriyu Atwubrisiyu mtunzi wa (Faslu al-khitwaabi…). Mashia wanalichukua jina hili kutokana na neno "taqiya" sio “taquwaa”. Na baba anayempa mwanawe anapozaliwa jina la taqiyu "anatarajia mwanawe atakuwa hodari mno katika taqiya na itikadi kinyume na anavyojidhihirisha kwa Waislamu.

wanazuoni wao. Kitabu hiki kinathibitisha kuwa wanazuoni hao wameamini na kukubali moja kwa moja hoja ya kuwa Quran imepotoshwa, lakini hawapendi kulipua zogo dhidi ya itikadi yao hii iliyo dhidi ya Quran.

Baada ya hayo kunabakia kitu kimoja nacho ni kuwa kuna Quran mbili ya kwanza inajulikana na watu wote na ya pili ni ya watu maalum na imefichwa, na ndani ya Qurani hiyo ya pili kuna surat "Al-Wilaaya". Kwa hiyo, hawa Mashia wanafundisha neno walilomtungia imamu wao Ali bin Al-Ridhwaa nalo ni "zisomeni kama mlivyojifunza, na atakujieni yule atakayekufunzeni".

Na kile Mashia wanachokidai kwamba katika Quran kumeondoshwa aya isemayo “Na tumemjaalia Ali kuwa mkweo”. Wamedai kwamba aya hiyo imetolewa kutoka katika sura “Alam nashraha”. Sura hiyo imeteremka Maka, na Ali hakuwa mkwe wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, alipokuwa Maka. Na hakika si jinginelo, katika kipindi cha Maka, aliyekuwa mkwe pekee wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, ni Al-Aaswi bin Al-Rabia Al-Umawiyi, Allah amuwie radhi, aliyesifiwa na Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, katika membari ya msikiti wa Mtume.

Ama Ali, Allah amuwie radhi, alitaka kumwoa binti wa Abuu Jahli dhidi ya Fatuma, Allah amuwie radhi. Fatuma akafichua jambo hilo kwa baba yake, Rehema na amani ziwe juu yake. Ikiwa Ali, Allah amuwie radhi, ni mkwe wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, kwa mmoja wa mabinti zake, tujue kuwa Allah Mtukufu, amemjaalia Athumani, Radhi za Allah ziwe kwake, awe mkwe wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, kwa mabinti zake wawili.

Binti wa pili wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, alipokufa, Mtume alimweleza Athumani, Allah amuwie radhi: “Kama tungelikuwa na binti wa tatu tungekuozesha”.

Mwanazuoni wa Kishia Abuu Mansuri Ahmad bin Ali bin Abuu Twaalibi Al-Twubrisiyu (mmoja wa mashehe wa ibnu Shahri Aashuubu aliyekufa mwaka 588 Hijiriya, katika kitabu chake ‘Al-Ihtijaaju Alaa Ahli Al-Lajaaji’) anadai kuwa Ali alimwambia mmoja wa wazandiki – hakumtaja jina: “Unavyojidhihirisha kwangu kwa kuipotosha kauli ya Allah Mtukufu isemayo (Na ikiwa mnaogopa kuwa hamtowafanyia mayatima uadilifu, basi oeni mnaowapenda katika wanawake…) Sura [4] An-Nisai.

Kwa hakika uadilifu kwa mayatima hauendani na kuwaoa wanawake. Na wanawake wote si mayatima. Haya ndio yale niliyotangulia kuyasema

kwamba wanafiki[3] wameondoa kutoka katika Quran maelezo yaliyokuwepo baina ya maneno yanayowahusu mayatima na kuwaoa wanawake. Na visa kama hivi vipo vingi vinazidi theluthi ya Quran”.

### Wanamuongopea hadi Ali, Allah amuwie radhi

Madai hayo ya kuondoshwa theluthi ya Quran ni miongoni mwa uongo wao wa kumsingizia Ali, Allah amuwie radhi, kwa ushahidi wa kwamba huyo Ali mwenyewe, wakati alipokuwa anatawala mambo ya Waislamu hajaitangaza hiyo theluthi iliyoondoshwa kutoka katika Quran na hasa hasa maudhui hii. Wala hajawaamrisha Waislamu waithibitishe hiyo theluthi au wafuate mwongozo wa theluthi hiyo wala hakuzifanyia kazi hukumu zake. (Pia tazama maudhui iliyopita – kuikosoa Quran Tukufu – kifungu cha mwisho na ufafanuzi wake wa pambizoni).

### Furaha ya Wahubiri wanaodai habari njema za Ukristo.

Kitabu (Faslu Al-Khitwaabi fii Ithibaati Tahriifu Kitaabi Rabbi Al-Arbaabi), kilipotoka na kusambaa kwa Mashia na watu wengineo huko Iran, Najafu na miji mingine kabla ya miaka minane na ushee iliyopita. Huku kitabu hicho kikiwa kimeshehenezwa makumi kwa mamia ya mifano ya uongo kama huu wa kumsingizia Allah na viumbe vyake vitakatifu. Wahubiri ambao ni miongoni mwa maadui wa Uislamu walikifurahia sana kitabu hicho na kukitafsiri kwa lugha zao.

Jambo hilo limetajwa na Muhammad Al-Mahdiyu Al-Aswifahaaniyu katika ukurasa wa 90 wa juzuu ya pili ya kitabu chake (Ahsanu Al-Wadiiati) na kitabu hiki ni kitoto cha kitabu chao (Rawdhwaatu Al-Jannaati). Katika Bukhari yao inayoitwa (Al-Kaafii) ya Al-Kiliiniyu kuna maandiko mawili ya wazi wazi. La kwanza lipo katika ukurasa wa 54 wa chapa ya Iran ya mwaka 1278. Andiko lenyewe ni:

"Kutoka kwa Jabiri Al-Jaafiyu amesema: Nimemsikia Abuu Jafari, Amani iwe juu yake, anasema: hakuna mtu hata mmoja aliyedai kuwa

---

[3]Abuu Mansuuri Al-Twubrisiyu anaowakusudia wanafiki kwa hapa ni Maswahaba wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, waliokusanya Quran. Na Ali bin Abuu Twaalibi, Allah amuwie radhi, wakati wa ukhalifa wake, aliifanyia kazi Quran iliyoandikwa na Athumani. Kama haya maneno aliyosingiziwa Ali katika kitabu cha Al-Ihtijaaju Alaa Ahli Al-Lajaaji’ yangekuwa kweli yametoka kwa Ali, Allah amuwie radhi, basi Ali angekuwa ameufanyia uhaini Uislamu kwa kuwa anajua kuwa kuna theluthi ya Quran iliyopotezwa naye kwa uchache haidhihirishi, wala haifanyii kazi wala hawaamrishi watu wapeane Quran hiyo wakati wa utawala wake. Hakukuwa na kizuizi chochote kinachomzuia Ali kutekeleza mambo haya, kwa hiyo kukificha kiwango hiki cha Quran huku akiwa ameridhia na kuuchagua unafiki kwa hiari yake. Kama ingekuwa sahihi kuwa Ali ndio msemaji wa upuuzi huu. Itakuwa Abuu Mansuuri Al-Twubrisiyu mtunzi wa kitabu ‘Al-Ihtijaaju’ kwa kitabu chake hiki anamtukana Ali mwenyewe na kumpa sifa ya uhaini na ukafiri kabla ya kuwatusi Maswahaba wa Mtume wa Allah na kuwapachika sifa ya unafiki.

ameikusanya Quran yote ispokuwa muongo. Na hakuna aliyeikusanya na kuihifadhi kama ilivyoteremshwa ispokuwa Ali bin Abuu Twaalibi na Maimamu wa baada yake".

Kila Mshia anayesoma kitabu hiki cha Al-Kaafii, kitabu ambacho umuhimu wake kwao ni sawa na Swahihu Bukhari kwetu sisi, analiamini andiko hili. Ama sisi Ahlu Sunna tunasema: (Kwa hakika Mashia wameongopa na kumsingizia Al-Baaqiru, Allah amrehemu. Kwa ushahidi wa kwamba Ali, Allah amuwie radhi, wakati wa ukhalifa wake huko Kufa hakuufanyia kazi msahafu wowote kinyume na Msahafu ambao Allah alimneemeshea nduguye Athumani, Allah amuwie radhi, kuukusanya, kuusambaza mijini, kuufanyia kazi kwa zama zote mpaka sasa, na mpaka siku ya Kiama.

Na kama Ali angekuwa na Msahafu mwingine usiokuwa huu uliopo huku Ali huyo huyo akiwa ni khalifa, kiongozi asiyepingwa na yoyote katika eneo la hukumu yake – angeufanyiakazi msahafu huo na kuwaamrisha Waislamu wauneze pamoja na kuufanyiakazi. Na kama angeuficha ili Waislamu wasiuone, basi angekuwa ni mwenye kufanya uhaini kwa Allah, kwa Mtume wake na kwa dini ya Kiislamu.

Jabiri Al-Jaafiyu, mtu wanayemdai kuwa ndio aliyesikia maneno hayo ya madhambi kutoka kwa Imamu Abuu Jafari Muhammad Al-Baaqiri, hata kama anaaminiwa na Mashia, lakini kwa maimamu wa Waisalamu wa madhehebu mengine mtu huyu ni maarufu kwa uongo. Abuu Yahya Al-Hamaaniyu amesema: nimemsikia Abuu Hanifa akisema: sijawahi kumwona mtu aliyembora kuliko Atwaa, na aliyemwongo kuliko Jabiri Al-Jaafiyu.

Andiko la uongo zaidi kuliko hili limo katika kitabu cha (Al-Kaafii) kutoka kwa Abuu Jafari. Hili ni andiko la pili alilosingiziwa mtoto wa Jafari Al-Swaadiqu. Andiko lenyewe kama lilivyo katika Bukhari yao (Al-Kaafii) pia limo kwenye ukurasa 57 chapa ya mwaka 1278 iliyochapishwa Iran, nalo ni:

"Kutoka kwa Abuu Baswiiru amesema: niliingia kwa Abuu Abdallah (yaani Jafari Al-Swaadiqu) akasema: “kwa hakika tuna Msahafu wa Fatuma, Amani iwe juu yake, … akasema: nikamuuliza, Msahafu wa Fatuma ndio nini? Akasema: huo ni Msahafu ndani yake mna Quran kama Quran yenu hii kwa mara tatu zaidi. Naapa kwa Allah, katika Quran yenu hamna hata herufi moja"!

Maandiko haya ya Kishia yanayowasingizia uongo maimamu wa Ahlu beiti ni ya zamani sana. Muhammad bin Yakubu Al-Kiliiniyu Al-Raaziyu

ameyasajili maandiko hayo katika kitabu chake (Al-Kaafii) kabla ya miaka elfu moja na zaidi. Na maandiko hayo ni ya zamani sana kumpita yeye mwenyewe kwani yeye ameyapokea kutoka kwa waliomtangulia miongoni mwa wanazuoni wa uongo *mainjinia* wa kuujenga Ushia.

Wakati Hispania ilipokuwa chini ya utawala wa Waislamu wa Kiarabu, Imamu Abuu Muhammad bin Hazmi alikuwa anajadiliana na kasisi wa Hispania kuhusu maandiko ya vitabu vyao. Aliwatolea hoja za namna walivyovipotosha na kupoteza vitabu vyao vya asili. Kasisi huyo akawa akitoa hoja kuwa Mashia wametoa azimio kuwa: Quran nayo imepotoshwa. Ibni Hazmi akawajibu kuwa madai ya Mashia sio hoja dhidi ya Quran, wala kwa Waislamu kwa sababu Mashia si Waislamu.[4]

**Rai ya Mashia kwa viongozi**

Ukweli wa hatari unaovuta macho ya serikali zetu za Kiislamu ni kuwa dhehebu la Kishia Al-Imaamiya Al-Ithnaasheria, pia linaitwa (Al-Jafariya), asili yake imejengeka kwa kuzizingatia serikali zote za Kiislamu tangu siku aliyofariki Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, mpaka sasa hivi – ukitoa miaka ya utawala wa Ali bin Abuu Twaalibu, Allah amuwie radhi – kuwa si za kisheria. Na Mshia hapaswi kuwatii wala kuwatendea kwa nia njema kutoka moyoni mwake viongozi wa serikali hizo. Ispokuwa anapaswa kuwapaka kiremba cha ukoka na kuwafanyia taqiya kubwa.

Kwa kuwa serikali zote hizo, sawa zilizopita, au zilizopo au zitakazokuja hapo baadaye ni serikali zilizopora uongozi. Viongozi wa kisheria katika dini ya Kishia na undani wa itikadi yao ni Maimamu kumi na wawili peke yao. Ni sawa sawa kwa Mashia, ikiwa Maimamu hao wafanikiwa kushika uongozi au hawakushika.

Na yoyote atakayekuwa si katika wao, miongoni mwa wale walioshika madaraka kwa maslahi ya Waislamu, kuanzia Abuu Bakri, Omari na walio baada yao mpaka sasa hivi, vyovyote walivyouhudumia Uislamu, tabu yoyote waliyoipata katika kuutangaza wito wa Kiislamu na kuliweka juu neno la Allah ardhini, na kupanua wigo wa ulimwengu wa Kiislamu. Watu hao ni waovu na wapora madaraka hadi siku ya kiama.

**Chuki dhidi ya Abuu Bakari na Omari**

[4]Tazama kitabu: Al-Faslu fii Al-Milali Wannihali, cha Ibni Hazmi juzuu 2 uk 182, chapa ya kwanza Cairo.

Kwa sababu ya chuki, Mashia wanawalaani Abuu Bakari, Omari na Athumani, Allah awawie radhi. Pia wanamlaani kila aliyeshika uongozi katika Uislamu ispokuwa Ali, Allah amuwie radhi. Wamemuongopea imamu Abuu Al-Hassan Ali bin Muhammad bin Ali bin Musa kuwa amewakubalia Mashia zake wawaite Abuu Bakari na Omari ‘Majibtu na Matwaghuuti’ yaani mashetani waovu.

Katika kitabu chao wanachokiitakidi kuwa ndicho kikuu na kikamilifu katika ‘jarhi wataadili’ kukosoa na kusahihisa hadihi. Kitabu hicho ni (Tanqihu Al-Maqaali fii Ahwaali Al-Rijaali – yaani Kusafisha yaliyosemwa kuhusu hali za watu), juzu ya kwanza uk 207 kilichochapwa katika kiwanda cha Al-Murtadhwiaya huko Najafu mwaka 1352 Hijiria.

Kitabu hiki kimetungwa na Sheikh wa kundi la Jaafariya, ambaye ni mwanazuoni mkuu wa pili akiwa na cheo cha Ayatullahi Al-Maamaqaaniyu. Kwa kutumia yale aliyoyanukuu kutoka kwa Sheikhe Mtukufu ambaye ni Muhakiki, Muhammad bin Idirisa Al-Halabiyu mwishoni mwa kitabu (Assaraairu) Kutoka katika kitabu (Masaailu Rijaali Wumakaatabatihimu ila Maulana Abuul Hassan Ali bin Muhammad bin Ali bin Musa Alayhi salaam).

Miongoni mwa mambo ya Muhammad bin Ali bin Issa amesema: Nilimwandikia kumuliza Sheikhe Muhammad bin Idirisa Al-Halabiyu juu ya mwenye kunasibishwa (yaani Yule anayenasibishwa na uadui kwa Aali baiti), je nikimfanyia mtihani nahitaji kingine zaidi ya kumpatia wale Jibti na Twaghuuti (yaani kumuuliza juu ya Mashekhe wawili ambao ni maswahaba na mawaziri wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yao nao ni Abu Bakri na Omari) kuhusu itikadi yake kuhusu uimamu wa wawili hao?

Jibu likaja hivi: Atakayekuwa na msimamo huo wa kuwakubali wawili hao, basi mtu huyo ni mwenye kuwafanyia uadui Aali baiti. Yaani, binanadamu inamtosha azingatiwe kuwa ni adui wa Aali baiti akiwatanguliza Abu Bakri Asswidiiq na Omari Al-Faaruqu na akaamini uimamu wao! Na maneno Jibti na Twaghuuti yanatumiwa na Mashia katika dua yao wanayoiita (Dua ya masanamu mawili ya Kikureyshi) wakiwakusudia Abuu Bakri na Omari.

Yaani Jibti na Twaghuuti: (Abuu Bakri na Omari). Dua hii ipo katika kitabu chao (Miftaahul Jinaani) uk 114 na kitabu hiki kina nafasi kama ya kitabu cha “Dalaailul khairaati” katika ulimwengu wa Kiislamu. Na andiko la dua yao hiyo ni: “Ewe Mola mswalie Muhammad na Aali wa Muhammad, na walani masanamu wawili ya kikureyshi na Jibti wao, na Twaghuuti wao na mabintia zao… hadi mwisho. Mabinti zao

wanaokusudiwa ni “Mama wa waumini Aisha na Mama wa waumini Hafswatu” Allah awawie radhi wote.

**Kumtukuza aliyemuua Omari**

Kwa sababu ya kuchukuia kwao, namna Omari alivyouzima moto wa Majusi huko Irani, na hiyo ndio ikawa sababu ya babu zao kuingia Uislamu, Mashia walimwita muuaji wa Omari ambaye ni Abuu Luuluu Mmajusi kwa jina la “Abuu Shujaa Ddini” yaani Shujaa wa dini.

Ali bin Mudhwaahiri, miongoni mwa Mashia, amepokea kutoka kwa Ahmad bin Is-Haqa Alqumiyu Al-Ahwaswi (Sheikh wa Kishia), amepokea kwamba: siku ya kuuawa Omari bin Alkhatwaabi, hiyo ni siku kuu kubwa sana, ni siku ya kujifaharisha, siku tukufu, ni siku ya utakaso mkuu, siku ya baraka, na ni siku ya kujiliwaza.

**Kikwazo cha Utawala**

Tangu kuanzia utawala wa Abuu Bakri, Omari, Swalahuddini Al-Ayuubiyu na wale wote walioukombolea Uislamu mamlaka za dunia na kuziingiza katika dini ya Allah. Na wale waliotawala kwa jina la Uislamu hadi kufikia siku yetu ya leo, wote hao, kwa mujibu wa itikadi ya Mashia watakayokutana nayo na Allah, ni watawala wanaotawala kwa mabavu na ni madhalimu, pia ni watu wa motoni. Kwa sababu watu hao hawajatawala kisheria wala hawakustahiki kupata utiifu au ushirikiano wa Mashia katika mambo ya heri ila kwa kiwango kile kinachokubalika katika itikadi yao ya “Taqiya” au kwa tamaa ya kupata vitu kutoka kwa watawala kwa njia ya kuwafanyia kinafiki.

Miongoni mwa itikadi zao za msingi ni kuwa: Imamu Mahdi (huyu ni Imamu wao wa kumi na mbili) ambaye kwa sasa yu hai kwa mujibu wa madai yao. Wanamngojea ajitokeze ili aanzishe mapinduzi akishirikiana na Mashia katika mapinduzi hayo. Mashia wanapomtaja Imamu Mahdi katika vitabu vyao wanaandika pembezeni mwa jina lake herufi mbili nazo ni (Aini na Jimu) yaani ni kifupi cha “Ajjil Jaliyuhu - Ewe Allah harakisha kutokea kwake”.

Wakati Imamu Mahdi atakapoamka kutoka katika usingizi wake mrefu ambao umeshavuka miaka elfu moja na mia moja. Allah atawafufua watawala wote wa Kiislamu waliopita na kuwaweka pamoja na watawala wa wakati huo wa kusimama kwake. Watawala hao watafufuliwa kwa ajili ya Imamu Mahdi na baba zake. Na watawala hao wataongozwa na Abuu Bakri, Omari na waliokuja baada yao – Kisha Imamu Mahdi

atawahukumu kwa kosa la kupora madaraka yake na madaraka ya baba zake ambao ni wale maimamu wa Kishia kumi na mmoja.

Kwa kuwa madaraka katika Uislamu ni haki ya maimau wa Kishia peke yao. Haki itokayo kwa Allah, tangu kufa kwa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, hadi kusimama kwa Kiama. Kwa hiyo, hakuna mtu yoyote asiyekuwa wao, mwenye haki ya kutawala.

Kisha, Imamu Mahdi baada ya kuwahukumu matwaghuti hao waliopora madaraka atawalipizia kisasi kwa kuamrisha kuuawa na kunyongwa watu mia tano pamoja na viongozi hao ili atimize kuua watu elfu tatu miongoni mwa watawala wa zama zote za Kiislamu. Na hayo yanatokea hapa duniani kabla ya ufufuo wa mwisho wa siku ya Kiama.

Kisha baada ya kufa watakaokufa na kunyongwa watakaonyongwa ndipo kutakapokuwa na huo ufufuo mkubwa katika siku ya kukusanywa watu, kisha watu wataingizwa peponi au motoni. Pepo ni ya Aali baiti na wale wanaoamini itikadi ya Aali baiti, na Moto ni wa kila asiyekuwa Mshia.

Mashia wanaiita mahakama hiyo, au ufufuo huo na kisasi hicho kwa jina la (Al-Raji`atu – Kurejea), na hii ni miongoni mwa itikadi yao ya msingi itikadi ambayo hakuna hata Mshia mmoja mwenye shaka nayo. Nimewaona miongoni mwa wale wenye mioyo mizuri wakidai kuwa itikadi kama hizi, Mashia wameshaziacha katika zama za hivi mwishoni. Na madai haya ni kosa kubwa linalopingana na uhalisia.

**Kutoka katika Ushia hadi Ukoministi**

Mashia tangu siku za Dola ya Kisufi hadi sasa wanazing`ang`ania itikadi za Kishia na Kisufi kuliko walivyokuwa hapo awali. Sasa hivi Mashia, ima wanaamini yote hayo, au wanajifunza mafunzo ya kisasa, kwa hiyo wamezikengeuka itikadi hizo za kihovyo hovyo na kujiunga katika itikadi za Kikoministi.

Ukoministi wa huko Iraq na chama cha TUUDA huko Iran vimetokana na kizazi cha Mashia ambao wameona hakika ya ngano za Kishia, kwa hiyo wakawa wakoministi badala ya Mashia. Na hakuna Mashia mwenye chama cha mlengo wa kati ila wale tu wanaojionesha hivyo kwa kutumia taqiya kwa malengo ya kimadhehebu, kidiplomasia, kichama au kibinafsi. Huku wakificha vile wasivyovidhihirishwa.

Ili uifahamu vizuri itikadi ya (Al-Raji`atu), kutoka katika vitabu vyao vinavyokubalika, nakutajia yale yaliyosemwa na sheikhe wa Kishia Abuu Abdallah Muhammad bin Muhammad bin Nouman, maarufu kwa Mashia

kwa jina la (Sheikh Al-Mufiidu) katika kitabu chake (Al-Irshaadu fii Ta`ariikhu Hujajillah Alaal Ibaadi) uk 398 – 402.

Kitabu hicho kimechapwa katika jiwe huko Irani kwa chapa ya kizamani, bila kutajwa tarehe ya kuchapishwa. Lakini pia, kikachapwa kwa hati ya Muhammad Ali Muhammad Hassan Al-Kalbaabakaatii. Imeandikwa: Al-Fadhli bin Shaadhaan amepokea kutoka kwa Muhammad bin Ali Al-Kuufiyu kutoka kwa Wahbu bin Hafswi, kutoka kwa Abuu baswiiru amesema: Abuu Abdallah (yaani Jafari Al-Swaadiqu) amesema: Pataitwa kwa jina la Aliyesimama (yaani imamu wao wa kumi na mbili wanayemdai kuwa amezaliwa zaidi ya karne kumi na moja zilizopita na bado hajafa, kwa kuwa atasimama na kuhukumu), kwa hiyo ataitwa kwa jina lake usiku wa ishirini na tatu.

Naye atasimama siku ya Ashuraa, kana kwamba mimi nipo pembeni yake, katika siku hiyo ya kumi ya mwezi wa Muharram Mfunguo nne, akiwa amesimama baina ya ile Nguzo na Maqaam. Huku Jibrilu akiwa kuumeni kwake anaita: Baiaya ya Allah. Mashia wa pande zote za dunia watamwendea wakimzunguka mzunguko mkubwa wakimbaiyi. Kuna athari iliyokuja inaeleza kuwa huyo Mahdi atatembea kuanzia Makka hadi Kufa na atafikia Najafu kisha atalitawanya jeshi liende kila mji.

Al-Hajalu amepokea kutoka kwa Tha`alaba bin Abuu Bakr Al-Hadharamiyu kutoka kwa Abuu Jafari, (yaani Muhammad Al-Baakiri) amani iwe juu yake amesema: Kana kwamba nipo kwa huyo Al-Qaaimu amani iwe juu yake, huko Najafu Kuufa naenda huko nikitokea Makka nikiwa na malaika elfu tano, Jibrilu yupo kuumeni kwake na Mikailu kushotoni mwake. Waumini wapo mbele yake huku yeye mwenyewe akilitawanya jeshi mijini.

Imepokewa kutoka Abdul Kariim Al-Ja`afiyu amesema: Nilimuuliza Abuu Abdallah (Yaani Jafari Al-Swaadiq) huyo Al-Qaaimu atakuwa kwa miaka mingapi? Akajibu miaka saba. Siku zitakuwa ndefu hadi mwaka mmoja miongoni wa miaka ya wakati huo utakuwa na urefu sawa na miaka kumi ya miaka yenu hii. Abuu Baswiiri akamwambia: nifanywe fidia yako, Allah atairefusha vipi miaka hiyo? Akasema Allh ataamrisha mbingu zikae na ziwe na mwendo mdogo.

Kwa hiyo siku zitakuwa ndefu pia miaka itakuwa mirefu. Na kudhihiri kwake kukikaribiwa watu watanyeshewa na mvua katika mwezi wa Mfunguo tisa na katika zile siku kumi za mwanzo za mfunguo kumi, mvua ambayo haijapatapo kuonwa na yeyote miongoni mwa viumbe, mvua kama hiyo. Allah ataotesha nyama za miili ya waumini kutoka

katika makaburi yao. Kana kwamba mimi ninawatazama wakiwa wanakuja huku wakikung`uta nywele zao kutoa vumbi.

Imepokewa kutoka kwa Abdallah bin Al-Mughiira kutoka kwa Abuu Abdallah (Yaani Jafari Al-Swaadiq) Amani iwe juu yake amesema: Atakaposimama huyo msimamaji miongoni mwa Aali Muhammad atawasimamisha Maqurayshi mia tano na kuzikata shingo zao kisha Maqurayshi miatano wengine anawakata shingo zao kisha atawasimamisha Maqurayshi mia tano wengine na anawakata shingo zao kisha atawasimamisha Maqurayshi mia tano wengine na anawakata shingo zao anafanya hivyo hadi mara sita.

Nikamuuliza: Je, idadi ya Maqurayshi hao itafikia hivyo? (Hakika si jinginelo, ameshangazwa na hilo kwa kuwa idadi ya makhalifa waongofu na wa Banii Ummaya na wa Banii Al-Abbasi na wengineo wote miongoni mwa watawala wa Kiislamu hadi kufikia zama za Jafari Al-Swaadiq hawafikii moja ya kumi ya idadi hii) Jafari Al-Swaadiq akasema: ndio watachinjwa viongozi na wale waliowafuata.

Na katika riwaya nyingine: Kwa hakika dola yetu ndio dola ya mwisho. Na Ahlu Bait hawatabakiwa na dola ispokuwa ile waliyoimiliki kabla yetu ili pale watakapoona mwenendo wetu wasije wakasema: Mkitutawala mtaendenda kama wanavyoenenda hawa.

Imepokewa kutoka kwa Jaabir Al-Ja`afiyu kutoka kwa Abuu Abdallah amesema: Atakaposimama msimamaji miongoni mwa Aali Muhammad atapiga ‘Fasaatwiitwu’ siku hiyo Quran itajulishwa kama ilivyoteremshwa[5] Itakuwa ngumu sana kwa wale walioihifadhi ile ya leo hii (Yaani ile ambayo watu wameihifadhi katika Msahafu wa Athuman kama ilivyokuwa katika zama za Jafari Al-Swaadiq, kwa kuwa Quran hiyo inatofautiana na hiyo nyingine kiuandishi).

Amepoke Abdallah bin A`jalaani kutoka kwa Abuu Abdallah Amani iwe juu yake amesema: Atakaposimama msimamaji miongoni mwa Aali Muhammad atawahukumu watu kwa hukumu ya Daudi. “Kivipi?” Imepokewa kutoka kwa Al-Faadhil bin Omari kutoka kwa Abuu Abdallah amesema: Watu mia saba na ishirini miongoni mwa kaumu ya Musa watatoka pamoja na huyo msimamaji Amani iwe juu yake katika maeneo ya Kuufa? Na watu saba miongoni mwa watu wa Kuufa, pia takuwep Yoshua bin Nuuni na Suleyman, Abuu Dajaanah Al-

[5] Kwa nini babu yake ambaye ni Ali bin Abuu Twaalib hakufanya hivyo wakati wa utawala wake? Je, mjukuu wake wa kumi na mbili ndio mwenye kuitendea haki Quran na Uislamu kuliko yeye mwenyewe??

Answaariyu, Al-Miqdaadi, Maaliki Al-Ashtari na watakuwa mbele yake wakiwa ni watu wanaomnusru nao ni watawala.

Maandiko haya yamenukuliwa neno kwa neno, na kwa uaminifu wote kutoka katika vitabu cha mwanazuoni mkubwa miongoni mwa wanazuoni wao wakuu naye ni Sheikh Al-Mufiidu. Pia zimepokewa na sanadi zake – na bila shaka – ni za uongo wa kuwasingizia Aali Baiti waliokuwa na msiba mkubwa wa kufuatwa na wafuasi wengi waongo. Vitabu vya Al-Mufiidu vimechapwa huko Iran na kopi yake ya kale kabisa ipo na imehifadhiwa.

## Itikadi ya Al-Raji`atu

Kwa kuwa itikadi ya Al-Raji`atu yaani kurudi kuwahukumu watawala wa Kiislamu ni miongoni mwa itikadi za msingi za Mashia. Mwanazuoni wao Assayidu Al-Murtadhwaa alikuwa akiiamini itikadi hii, akatunga kitabu (Amaaliyu Al-Muratadhwaa). na ndugu yake ambaye ni Al-Shariifu Alridhwaa Asshaai‘ru naye alikuwa mwenziwe katika kupotosha na kuweka ziada za (Nahjul Balaagha). Huenda kitabu hiki kimepotoshwa zaidi ya theluthi yake na ziada hiyo ndio yenye kuwashutumu Maswahaba na kuwalaani.

Huyu Assayidu Al-Murtadhwaa aliyetajwa hapa amesema katika kitabu chake hiki (Al-Masaailu Annaaswiriyati): Kwa hakika Abuu Bakri na Omari watasulubiwa katika siku hiyo juu ya mti wakati wa zama za Al-Mahdiyu (Yaani imamu wao wa kumi na mbili wanayemwita msimamaji miongoni mwa Aali Muhammad) mti huo utakuwa mbichi kabla kusulubiwa kisha utakauka baada ya kuwasulubu.

## Fikra zao hazijabadilika

Matangazo na habari za Kishia katika zama zote zipo katika msimamo huu wa kuwaudhi Maswahaba wakuu wawili wa Mtume wa Allah, ambao ni mawaziri wake Abuu Bakri na Omari. Vilevile kuwaudhi wakuu wote wa Kiislamu miongoni mwa makhalifa, watawala, viongozi na, mujahidina na waliohifadhi Quran. Tumeshamsikia mlinganiaji wao aliyesimamia Daaru Attaqriibi anayoilipia akidai kwa wale wasio na wakati wa kuyasoma mambo haya, kuwa itikadi hizi zilikuwa katika zama za waliotangulia na kwa sasa hali imeshabadilika.

Madai haya ni uongo mtupu na khidaa, kwani vitabu vinavofundishwa katika vyuo vyao vyote vinafundisha kuwa mambo hayo ni ya lazima kwa madhehebu yao pia ni nukta za msingi, na vitabu vinavyosambazwa na wanazuoni wa Najafu, Iran na Jaalu Aamili. Na katika zama zetu hizi

ndio kuna ubaya zaidi wenye kuangamiza zaidi matamanio ya kukurubiana na kufahamiana kuliko zama za vitabu vyao vya kale.

Tunakupigia mfano wa jambo hilo kwa mmoja wao ambaye aliendelea kutangaza kila siku asubuhi na mchana kuwa yeye ni mlinganiaji wa umoja na kukurubiana, naye si mwingine ila ni Sheikh Muhammad bin Muhammad Mahdiyyu Al-Khaaliswiyu, mwenye marafiki wengi huko Misri, na wengineo miongoni mwa wanaodai kuwepo kwa kukurubiana na wanafanya kazi hiyo baina ya Ma-Ahlu Sunna.

Mlinganiaji huyu wa kukurubiana na kufahamiana amefikia upeo wa kupinga neema ya imani kwa Abuu Bakri na Omari, pale aliposema katika kitabu chake (Ihyaau Shariiati fii Madh-habi Shiiati) juzuu ya kwanza ukurasa wa 63 – 64. “Wakisema kwamba Abuu Bakri na Omari ni miongoni mwa watu wa Baiatu ridhiwaani, watu ambao wameteremshia andiko la kuridhiwa katika Quran pale iliposema: “Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewapa radhi Waumini walipofungamana nawe chini ya mti, na alijua yaliyo moyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawalipa kwa Ushindi wa karibu”. Sura [48] Al-Fath 18.

Tunasema: Kama ingesemwa amewaridhia wale ambao wamekubaiyi basi aya hiyo ingekuwa ni ushahidi wa kuridhiwa wale wote waliombayi lakini kwa kuwa Allah amesema “Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewapa radhi Waumini walipofungamana nawe chini ya mti” kwa hiyo aya hii si ushahidi wa kuridhiwa kwao ispokuwa aya hii ni ushahidi wa kuridhiwa waumini peke yao?!

Kwa maana hiyo Abuu Bakri na Omari hawakuwa waumini kwa hiyo aya hii haiwahusu na hawana radhi za Allah!... Kabla ya madai haya tumeshatanguliza yale aliyoyasema Najafiyu mtunzi wa kitabu “Azzahraau” kumuhusu Omari bin Alkhatwaabi ya kwamba Omari amepewa gonjwa lisilopona ila kwa maji ya wanamume!! Hawa ni wanazuoni wawili wa Kishia wa kisasa tunaoishi nao, pia hawa ndio wale wenye wito mrefu na mpana wa uchungu na Uislamu na Waislamu, pia wanapupia mema na maslahi ya Uislamu na Waislamu.

Sasa ikiwa haya ndio wanayoyakariri katika vitabu vyao vya kisasa vilivyochapwa na kusambazwa, vitabu vinavyoeleza itikadi zao juu ya Abuu Bakri na Omari. Wakati Abuu Bakri na Omari ni Waislamu bora zaidi baada ya Mtume wa Allah, Rehema na amani ziwe juu yake, au kwa uchache, wao ni miongoni mwa Waislamu bora katika historia ya Uislamu kwa upande wa MAsunni.

Sasa kama ni hivyo, watu kama sisi, unatutarajia kuwa tutapata matumaini gani ya kufahamiana na kuitikiana ili kukaribiana kwa madhehebu?! Kwa hakika hawa wote si lolote ila ni mstari wa tano (mstari wa tano maana yake ni watu wanafiki na ndumila kuwili) katika ngome ya Waislamu?! Pale wanapowashusha Maswahaba wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, na waliowafuata wao kwa wema, pia kuwashusha viongozi wote wa Kiislamu wa baada yao hadi kufikia upeo huu unaosikitisha.

Lakini pia watu hawa hawa wanaowatukana ndio waliousimika Uislamu kiwazi wazi. Mashia hao hao wanawadai maimamu zao mambo yanayokataliwa na maimamu zao wenyewe. Alkiliniyu amesajili katika kitabu chake (Al-kaafi), sifa za Maimamu kumi na wawili zinazowanyanyua kutoka ubinadamu hadi kufikia nafasi kuabudiwa kama ibada ya Kiyunani katika zama za kuabudu masanamu. Na kama tungetaka kuyanukuu hayo kutoka katika (Al-kaafi) na vitabu vyao vingine vinavyotegemewa kwao ambavyo ni vya nafasi ya kwanza, tungejaza mjeledi mkubwa mno.

Kwa hiyo tunatosheka na kunukuu anuani za milango tu kama zilivyoandikwa kutoka katika kitabu (Al-kaafi) miongoni mwazo ni: “Mlango – kwa hakika maimamu wanajua elimu zote zilizotoka na kwenda kwa Malaika na Mitume na Manabii”. Mlango – kwa hakika maimamu wanajua watakufa lini na hawafi ila kwa hiari zao”. Mlango – kwa hakika maimamu wanajua elimu ya vilivyokuwepo na vitakavyokuwepo na wao hawafichikiwi na kitu. Mlango – kwa hakika maimamu wanavitabu vyote, wanavijua kwa lugha tofauti tofauti”.

Mlango – hakuna aliyeikusanya Quran yote ispokuwa Maimamu, na hao maimamu wanajua elimu ya Quran yote”. Mlango – yale yaliyo kwa Maimamu miongoni mwa alama za Mitume”. “Mlango – amri ya Maimamu ikidhihiri watahukumu kwa hukumu za Daudi!? Na watu wa Daudi!? Wala hawatauliza ushahidi”. Mlango – hakuna kitu cha haki kwa watu wote ispokuwa kile kitokacho kwa Maimamu na kwamba kila kitu kisichotoka kwa Maimamu, kitu hicho ni batili” Na mlango – kwamba ardhi yote ni ya Imamu.” [6]

**Kujificha kwa Maimamu!!**

Mashia wanadai kuwa Maimamu zao kumi na wawili wana vitu ambavyo hata hao Maimamu wenyewe wanavikana. Wanadai kwamaba Maimamu zao wanajua elimu ya ghaibu (iliyofichikana), pia hao Maimamu ni zaidi

[6] Tazama Al-Kaafii uk 225 – 407

wanadamu wa kawaida, wakati Mashia hao hao wanampinga Mtume SAW juu ya kile alichofunuliwa na Allah miongoni mwa mambo yaliyofichikana, kama masuala ya kuumbwa kwa mbingu na ardhi na sifa za Peponi na Motoni.

Madai hayo yamesajiliwa na jarida la (Risaalatul Islaam – Ujumbe wa Kiislam) linalotolewa na Darul Taqriibi huko Cairo. Katika toleo lake la nne la mwaka wa nne, ukurasa wa 368, makala liyoandikwa na rais wa Mahakama Kuu ya Sheria za Shia huko Lebanoni, na huyu anatambulika kuwa ni miogoni mwa wanazuoni wao wakubwa kabisa wa zama hizi aliandika makala isemayo: (Miongoni mwa ijitihaadaati za Mashia Imaamiya).

Katika makala hayo amemnukuu Mujitahidi wao ambaye ni Sheikh Muhammad Hassan Al-Ashtiyaaniyu, akisema katika kitabu chake (Bahru Alfawaaid) juzuu ya 1 ukurasa wa 267: Ya kwamba, Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, ikiwa ataeleza habari za hukumu za kisheria yaani mfano vitengua udhu na hukumu za hedhi na nifasi – lazima tuzisadikishe na kuyafanyia kazi yale aliyoyaeleza.

Ama akieleza mambo ya ghaibu kama kuumbwa kwa mbingu na ardhi, mahuru aini na makasri, haipasi kufuata dini kwa vitu hivyo baada ya kuvijua (yaani baada ya kujua usahihi wa kuwa zimetoka kwa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake) ama zile za kudhani tu ndio hazichukuliwi kabisa.

**Ajabu ilioje!!**

Mashia wanawasingizia uongo Maimamu zao, na kuwanasabisha na elimu ya ghaibu, na kuamini hilo. Wakati amabapo swala la kuwanasibisha Maimamu na elimu hiyo si suala lililothibiti kwa ushahidi wa kukata usio na shaka. Wakati huo huo, wanajihalalishia kutolazimika kufuata dini kwa habari za ghaibu zilizosahihi kutoka Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, tena kwa ushahidi wa kukata kabisa, kama vile Aya na Hadithi Sahihi zinazohusiana na kuumbwa kwa mbingu na ardhi, sifa za Peponi na Motoni.

Wanazikataa habari hizo za Mtume, licha ya kuwa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, hatamki kwa matamanio ya nafsi yake kwa kila ailichokieleza, kwa kuwa yeye hafuati ila ufunuo unaofunuliwa kwake.

Mtu atakayelinganisha baina ya kile walichowanasibishia Maimamu zao, na kile kilichosahihi kuwa kimetoka kwa, Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, miongoni mwa mambo ya ghaibu, atagundua kuwa yale

yaliyothibiti kutoka kwa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, katika Quran na Hadithi Mutawaatira na Sahihi hayafikii hata sehemu ndogo ya yale waliyowadaia Maimamu zao kumi na wawili, ya kwamba wana elimu ya ghaibu baada ya kukatika kwa ufunuo (wahyu) wa Allah ardhini.

Wapokezi wote wa riwaya za mambo ya ghaibu yanayowahusu Maimamu wa Kishia ni watu wanaojulikana na wanazuoni wa kubaini udhaifu na uadilifu wa wapokezi. Kitaalamu wanaita (jerhi wataadili) miongoni mwa Ahlu Sunna, kuwa wapokezi hao walikuwa waongo. Lakini wafuasi zao miongoni mwa Mashia hawajali suala hilo, na wanaendelea kuwasadikisha kwa kile walichokipokea miongoni mwa mambo ya ghaibu kutoka kwa Maimamu zao.

Wakati ambapo jarida la (Risaalatul Islaam – Ujumbe wa Kiislam) linalotolewa na Darul Taqriibi Cairo, na Kadhi wa mahakama yao ya Sheria za juu huko Lebanoni na Mjitahidi wao (Muhammad Hassan Al-Ashtabaaniyu) wanapiga makofi na kushangilia wito wa kutomsadikisha Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, kwa yale mambo yaliyosahihi kutoka kwake miongoni mwa mambo yaliyofichikana. Na hiyo ni kutaka kuifunga kazi ya Ujumbe wa Mtume Muhammad katika maswala ya kutengua udhu, hukumu za hedhi na nifasi na yale yanayofanana na hayo tu miongoni mwa matawi ya kifiqihi.

Wakati huo huo Mashia wanavikuza vyeo vya Maimamu zao katika mambo ya ghaibu hadi kuvizidi vyeo vya Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake. Licha ya kuwa huyu Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, ndiye aliyekuwa akifunuliwa wahyi. Huku hao Maimamu hawajadai hata mara moja kuwa wanapata wahyi. Kwa hiyo, hatujui kukaribiana gani kutakakoweza kuwepo kati yetu na wao baada ya mambo haya?!!

## Unafiki na kujikombakomba

Jambo lililofanyiwa uchunguzi katika vyanzo vyote vya kihistoria kwa Mashia wa ngazi za juu na za kawaida, kuhusiana na uhusiano uliopo baina yao na Viongozi wa serikali katika serikali za Kiislamu. Umebaini kwamba serikali yoyote ya Kiislamu itakapokuwa na nguvu na kuota mizizi, Mashia wanajikombakomba kwake kwa ndimi zao wakiwa wanaifanyiakazi itikadi ya “Al-Taqiya” ili wazinyonye heri za serikali hiyo na kuzikalia nafasi za serikali hiyo. Na iwapo serikali hiyo itadhoofika, au kushambuliwa na maadui, Mashia wataegemea katika swafu za adui na kuibadilikia serikali hiyo.

Hivyo hivyo ndivyo walivyokuwa mwishoni mwa Dola ya Umawiya. Pale Banuu Abbasi ambao ni watoto wa ami yao walipoleta machafuko, lakini machafuko ya Abbasiyiina yalikuwa yakipitia njia ya Mashia na kuwachonganisha na kuwapandikiza. Kisha katika hali kama hii Mashia wakawa waovu kwa dola la Bani Abbasi vilevile. Na pale dola la Bani Abbasi lilipotishiwa na kushambuliwa na Hulaako, na Maghuli wanaobudu masanamu.

Hiyo ilikuwa pale Hulaako, na Maghuli walipotaka kuungamiza utawala wa Kiislamu, mji mkuu wake Aazah, na kituo cha chake cha maendeleo ya kielimu.

Kisha Mashia wakawa na msimamo huo huo wa uovu pale kiongozi wao na mwanazuoni wao Al-Naswiiru Al-Twuusiyyu alipotunga shairi la kumsifu khalifa wa Abbasiya ambaye ni Muutaswim, wala haukupita muda mrefu akabadilika, mnamo mwaka 655 Hijiriya, akiwa anachochea uasi dhidi ya Muutaswim, huku akiharakisha kutokea janga kwa Uislamu huko Baghdad. Kisha akaja huku akiwa mstari wa mbele katika kikosi cha mmwaga damu Hulaako.

Baada ya hapo akafanyakazi ya kusimamia na kuhalalisha kuchinjwa (kufanyika kwa mauaji ya kimbari) kwa halaiki ya Waislam wanaume, wanawake, watoto na wazee. Yeye akiwa pamoja na Hulaako. Pia akaridhia kuzamishwa vitabu vya elimu vya Kiisalamu katika mto Digla hadi maji yake yakawa yanatiririka rangi nyeusi kwa siku nyingi, mchana na usiku, kutokana na wino wa vitabu ulioandikiwa vitabu hivyo.

Kwa hiyo urithi muhimu wa Kiisalamu ukatoweka. Miongoni mwa urithi huo ni vitabu vya historia, sanaa, lugha, mashairi na hekima. Pia elimu za sheria, na vitabu vya wanazuoni wa Kisalafi wale kizazi cha kwanza, navyo vikatoweka. Vitabu ambavyo vilikuwepo kwa wingi wakati huo, vikaharibika pamoja na vile vilivyoharibika miongoni mwa vitabu kama hivyo. Hilo ni janga la kiutamaduni, janga amabalo halijawihi kuwa na mfonowe.

**Usaliti (uhaini) wa Al-Qamiyu na Ibnu Abuu Al-Hadiidu**

Marafiki wawili wa sheikh wa Kishia bwana Al-Nasri Al-Tuusiyu walishirikiana naye kutenda uhaini mkubwa. Marafiki hao ni: Waziri wa Kishia ndugu Muhammad Ahmad Al-Alqamii na mwingine ni mtunzi wa anayefuata madhehebu ya Muutazila ambaye ni sheikh Abdulhamiid Alhudaid msaidizi mkuu wa Al-Alqamii. Bwana huyu Al-Nasri Al-Tuusiyu alikuwa ni adui mkuu wa Maswahaba wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, ndio maana akajaza uongo ulioupotosha historia ya

Uislam katika sherehe yake mbaya kabisa ya kitabu cha Nahju Albalaagha.

Watu wengi wasiojua historia ya kweli ya Kiislamu na hawajui vitu vilivyochomekewa, wanahadaika na maelezo yake. Cha kusikitisha zaidi ni kuwa, hadi watu werevu na watunzi wetu nao wamehadaika. Huyu Ibnu Alqamiyu aliyefanya uhaini huo alisamehewa na Khalifa Almuutaswimu kisha akakirimiwa na kupewa uwaziri. Lakini mapenzi ya uhaini na uovu uliokuwa nayo yalilipa wema aliotendewa kwa maovu.

La kusikitisha ni kuwa, Mashia hadi wa zama hizi wanafurahia janga la Huulako lililowakumba Waislamu. Ukipenda soma maelezo ya Mshia Nasri Altuusiyu katika vitabu vyake vyote vya maelezo ya watu muhimu alivyovitunga. Kitabu cha mwisho kabisa kiniatwa (Raudhaatu Aljannaati) cha Alkhuunsaariyu, kitibu hiki kimejaa sifa za kuwasifu waovu na wahaini, pia kinaonesha shangwe na furahia za kufurahishwa na janga lililowapata Waislamu.

Pia kitabu hicho kinaonesha namna anavyohisi raha pale wanapowaona wahanga wa Kiislamu wakipukutika. Pia wanafurahia mno namna Waislamu wanaume, wanawake, watoto na wazee walivyochinjwa. Wakati ambapo hata maadui wakuu wa Waislamu wanaona kinyaa juu ya mauaji hayo.

**Mashia wanatofautiana na Waislamu katika misingi ya dini, na si katika matawi tu.**

Ingawa nimejaribu kufupisha mada hii kwa kutumia Maandiko ya kutegemewa kutoka katika vitabu vya Mashia tu hata hivyo imerefuka. Sasa tuimalize kwa andiko lingine linalohusiana na mada hii ya kukurubiana ili kila Muislamu ajue kuwa kuna uwezekano wa kukurubiana na watu wa madhehebu mengine si Mashia na hilo linatokana na kukiri wazi wazi kwa Mashia. Tazama maelezo yafuatayo:

Alkhuunsaariyu amenukuu kutoka kwa mtaalamu wa historia wa Kishia katika kitabu chake (Raudhaatu Aljannaati) ukurasa wa 579, toleo la pili la Tehran, mwaka 1367 Hijiriya, maelezo ya Nasri Altuusiyu akieleza kuwa: miongoni mwa maneno yake ya ukweli na mazuri yatokayo kwa Mkweli wa haki na kwa kuhakikisha kauli yake ya kulianisha kundi litakalookoka katika yale makundi sabini na matatu, akadai kuwa kundi hilo ni kundi la Imaamiya, akasema:

“Nimeyafuatilia madhehebu yote na kuyajua hali zake na matawi yake, nikagundua kuwa madhehebu yote yasiyokuwa Imamiya yanashirikiana

hali zao na imani zao ijapokuwa wanatofautiana kwa baadhi ya mambo ambayo hayana tofauti kiimani  kama yatathibitishwa au yatakanushwa. Kisha nikagundua kuwa kundi la Imamiya linatofautiana na madhehebu yote kimisingi. Na kama kuna kundi miongoni mwao litaokoka basi makundi yote yataokoka, kwa hiyo hili linajulisha kuwa kundi litakalookoka ni Imaamiya tu na si linginelo.

Alkhuunsaariyu amesema: Bwana Neematullahi Almuusawiy amesema: Baada ya kuinakili ibara hii "uchambuzi wake ni kuwa, makundi hayo yanakubali kuwa Shahada mbili pekee ndio njia ya uokovu, wakiitafsiri kauli ya Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake: "Atakayesma Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah ataingia peponi".

Ama kundi la Imamiya wao wanaona kuwa hakuna uokovu ila kwa wilaya ya Ahli baiti hadi imamu wa kumi na mbili na kujitakasa na maadui zao (yaani Abuu Bakri, Omari na hadi mtu wa mwisho anayejinasibisha na Uislamu akiwa si Mshia, sawa sawa awe kiongozi au mfuasi wa kawaida). Kundi la Imaamiya linatofautiana na makundi mengine katika itikadi hii, ambayo ndiyo msingi wa uokovu".

Kwa hapa tunaona kuwa Atuusiyu, Almuusawiyu na Alkhuunsaariyu wamesema kweli na uongo kwa wakati mmoja. Wamesema ukweli pale waliposema kuwa makundi ya Waislamu yanakurubiana katika misingi ya dini na kutofautiana katika mambo ya matawi. Kwa hiyo kuna uwezekano wa kufahamiana na kukurubiana kwa makundi yaliyokurubiana kimisingi, na haiwezekani kufahamiana na Mashia Imamiya kwa kuwa kimsingi wanatofautiana na makundi yote ya Waislamu wala halimridhii Muislamu yeyote hadi atangaze kuwa Abuu Bakri, Omari na waliochini yao ni Majibti na Matwaghuuti (mashetani wakuu wanaoabudiwa) hadi siku ya kiama.

Pia Mashia wanapaswa wajitakase na kujitenga na kila asiye Mshia hata kama atakuwa na Aali Baiti miomgoni mwa mabinti wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake. Wanapaswa wajitakase na mabinti wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, waliolewa na Athumani bin Afaani, Bwana Alshahmu Al-Umawiyu Alnabiili Al-Aswi bin Rabiiu aliyesifiwa na Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, katika membari ya Msikiti mbele za Waislamu wote. Hilo lilijiri pale Imamu Ali alipotaka kumwoa binti wa Abuu Jahli na Fatuma akamshitakia baba yake juu ya jambo hilo.

Pia huko kijitakasa na kujitenga kunamuhusu Zaydi bin Ali "Zeini Al-Abidiina" bin Husein bin Ali bin Abuu Twalibu na Aali Baiti wengine waliokataa kujiunga na itikadi zilizopinda za RAAFIDHA (Mashia). Miongoni mwa itikadi hizo ni kudai kuwa Quran imepotoshwa. Wamedai

hivyo katika zama zote na katika matabaka yao yote kwa ushahidi wa yale yaliyonukuliwa na Mtaalamu wao, kipenzi cha mioyo yao, Alhaji Mirza Husein bin Muhammad Taqiyu Alnuuriyu Atwibrisiyu katika kitabu chake (Faslu Al-Khitwaabi fii Ithibaati Tahriifu Kitaabi Rabbi Al-Arbaabi).

Kwa hakika bwana huyu amechuma dhambi kubwa ya kuandika kila mstari akiwa pembezeni mwa kaburi la Swahaba mtukufu wa daraja ya amiri wa Kuufa bwana Almughiiratu bin Shuubatu, Allah amuwie radhi. Mashia wanadai kuwa kabri hili ni la Imamu Ali Bin Abuu Twaalibu Allah amuwie radhi.

Mashia wanatuwekea masharti ya kabla ili kukurubiana nao. Na ili waridhie kukurubiana na sisi: lazima sisi tutangaze pamoja nao kuwa tunatengana na Maswahaba wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, pia tujitenge na kila asiye Mshia hata akiwa binti wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, au tujitenge na wale wabora miongoni mwa kizazi chake, wakiongozwa na Zaydi bin Zeini Al-Abidiina na wale wote wanaoenenda mwenendo wake wa kupinga matendo ya Mashia.

Huu ndio upande wa kweli katika andiko hili lililonukuliwa kutoka kwa Annasri Altuusiyu, akafuatwa na Bwana Neematullah Almuusawiy, Mirza Muhammad Baaqiri Almuusawiy, Alkhuunsaariyu Al-Aswifahaaniyu. Na hakuna Mshia yeyote anayewahalifu hawa katika kauli hii kuanzia wale wanaozihirisha Taqiya hadi wale wanaojificha nayo.

Ama uongo waliousema ni madai yao ya kuwa kule kutamka shahada mbili tu ndio msingi wa uokovu huko Akhera, kwa wale wasio Mashia miongoni mwa Waislamu wengine. Kama wangekuwa na akili au ujuzi wangejua kuwa shahada mbili kwetu sisi ni anuani ya kuingia Uislamu, na atakayezitamka – hata akiwa anapigana vita kuupinga Uislamu – anakingwa damu na mali yake hapa duniani, ama kuokoka huko akhera kunaambatana na imani, na iamani ina ukamilifu wake.

Amiri muuminiina Omari bin Abdulazizi amesema: “Faradhi, Sheria, Hududi, na Sunna, atakayezikamilisha amekamilisha imani na asiyeikamilisha hajakamilisha Imani”. Kwa hiyo katika misingi ya Kissuni hakuna kule kusadikisha kuwepo kwa huyo Imamu wao wa kumi na mbili, kwani imamu huyo ni kitu cha kubuni tu kilichopachikwa kwa uongo kwa Hassan Al-Askariyu” aliyekufa akiwa hana mtoto, hata nduguye ambaye ni Jafari amemuelezea kuwa alikufa bila kuacha motto.

Pia kundi la Maalawiyiini wa wakati huo walikuwa na daftari la kudumu la kuorodhesha kila anayezaliwa, lakini hawajamworodhesha mtoto wa Hassan Al-Askariyu. Maalawiyiini wa zama za Hassan Al-Askariyu hawatambui kama Hassan Al-Askariyu aliacha mtoto wa kiume. Lakini huyo Hassan Al-Askariyu alipokufa akiwa hana mtoto, Mrorongo wa Uimamu ulisimama kwa wafuasi wa Imamiya, wakaona kuwa madhehebu yao yamekufa kwa kifo cha Hassan Al-Askariyu na wameshakuwa sio Maimamiya tena kwa kuwa hawatakuwa na Imamu mwingine.

**Kujitenga kwa Annaaswiriya na habari za njia ya chini ya ardhi.**

Shetani miongoni mwa mashetani zao aitwaye "Muhammad bin Naswiiru" ambaye ni miongoni mwa watumwa waliochawa huru na Banii Numairi aliutunga uongo wa kuwa Hassan Al-Askariyu ana mtoto aliyejificha katika njia ya chini ya ardhi ndani ya nyumba ya baba yake.[7] Aliutunga uongo huo ili yeye na wenzake, wawafanyie hila Mashia wa kawaida na wale Matajiri kwa lengo la kukusanya zaka kutoka kwao kwa jina la imamu huyo. Pia walikuwa na lengo la kuendeleza madai ya uongo ya kuwa wao ni Imaamiya.

Bwana huyu alitaka yeye mwenyewe awe ndiye mlango wa njia hiyo ya chini inayodaiwa, ili awapitishe Mashia wakakutane na imamu wao. Naye asimamie ukusanyaji wa mali ya zaka. Kuona hivyo wale wenzake aliotunga nao uongo huo, walitofautiana naye na wakang`ang`ania kuwa mlango uwe kwa muuza mafuta au samli, au uwe katika mlango wa duka ulio katika nyumba ya Hassan Al-Askariyu. Na watu wa Hassan Al-Askariyu na baba yake wakawa wanachukua mahitaji yao ya nyumbani kutoka kwa huyo muuza mafuta.

Hitilafu hiyo ilipotokea, yule mzushi wa uongo huu alijitenga na wenzake na akaanzisha dhehebu la Nnaaswiriya. Na wale wenzake wakatafuta njia ya kumdhihirisha huyo imamu wao wa kumi na mbili wanayedai kuwa yupo. Wakataka aoe ili awe na watoto kisha wajukuu waje kushika Uimamu na kuliendeleza dhehebu lao. Lakini wakagundua kuwa wakimdhihirisha tu, Maalawiyiina wote na ndugu zao ukoo wa makhalifa wa Banii Abbasi watamjua kuwa ni wa uongo.

Kwa hiyo wakadai kuwa imamu huyo amejificha katika njia ya chini ya ardhi, na huko ni kujificha kudogo. Ama kujificha kukubwa kutatokea

7Hiyo ni njia ya chini ya ardhi ndani ya nyumba ya baba yake – hata kama njia hiyo ya chini ilikuwepo – basi ilikuwa haiwahusu wao, wala hawana haki ya kuingia nyumba hiyo, kwa kuwa ni haki ya Jafari ndugu wa Hassan Al-askariyu. Na huyu Jafari anasisitiza kuwa Hassan Al-askariyu hana mtoto si ndani ya njia ya chini ya ardhi wanayoidai wala nje yake.

mwishoni mwa ngano (kisa) hii ambayo haijapatapo kusikiwa hata katika ngano za Wayunani (Wagiriki).

Kisha Mashia hao hao wanawataka Waislamu wote walioneemeshwa na Allah wakawa na neema ya akili waukubali uongo huu ili tu waweze kukurubiana na Mashia. Kwa kweli jambo hilo lipo mbali mno! Labda ulimwengu wote wa Kiislamu ubadilike na uende ukakae "Maaristaani" hospitali ya kutibu wagonjwa wa akili.

Sifa njema ni za Allah kwa kutupatia neema ya akili, kwani hiyo akili ndio kiini cha sisi kubebeshwa majukumu. Pa akili inazingatiwa kuwa ndio neema ya pili baada ya neema ya imani.

**Kuelemea upande wa Waislamu**

Waislamu wanaelemea upande wa kila Muislamu mwenye imani sahihi wakiwemo Aali Baiti wema, bila ya kikomo cha idadi maalum. Na miongoni mwa viongozi wa mstari wa mbele kuelemea upande wao ni: wale Maswahaba kumi waliobashiriwa pepo na Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake. Hata kama Mashia hawana sababu ya kuwakafirisha Maswahaba hao zaidi ya kumpinga Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, pale aliposema kuwa Maswahaba hawa kumi ni watu wa peponi.

Pia Waislamu wanaelemea upande wa Maswahaba wote waliobakia ambao wameusimika Uislamu. Pia wanaelemea upande wa uliwengu wote wa Kiislamu. Heri na haki iliyopo katika nchi za Kiislamu imepatikana kupitia damu zao. Maswahaba hawa ndio waliowakadhibisha Mashia walipodai madai mengi kumuhusu Ali na watoto wake. Kisha Mashia wakadai kuwa watu hawa ni madui wa Ali, wakati kwa hakika watu hawa waliishi na Imamu Ali kwa udugu, walipendana na kusaidiana.

Ni kweli kabisa sifa walizosifiwa na Allah Mtukufu katika surati Alfatihi aya 29 katika kitabu chake kisichoingiwa na batili, pale aliposema: "Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na waliopamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao..." Na kauli ya Allah katika surati Alhadiidi aya ya 10 (Na mna nini hata hamtoi katika Njia ya MwenyeziMungu, na hali urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa miongoni mwenu wenye kutoa kabla ya Ushindi na wakapigana vita. Hao wana daraja kubwa zaidi kuliko wale ambao waliotoa baadae na wakapigana. Na wote hao Mwenyezi Mungu amewaahidia wema. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za

mnayoyatenda). Allah akawataja tena katika surati Aali Imraan aya ya 110. (Nyinyi mmekuwa umma bora mmetolewa kwa watu…)

**Mapenzi baina ya Makhalifa waongofu**

Miongoni mwa mapenzi ya Amiri muuminiina Ali bin Abuu Twaalibu, Allah amuwie radhi, kwa ndugu zake Makhalifa watatu waliomtangulia ni kule kuwapa watoto zake waliozaliwa baada ya Mahasani wawili na Ibni Hanafiya, majina ya Makhalifa hao. Kwa hiyo tunakuta miongoni mwa watoto wa Ali kuna aliyempa jina la (Abuu Bakri) mwingine (Omari) na wa tatu (Athumani).

Pia Ali alimwozesha binti yake mkubwa, Ummu Kulthuumi kwa Omari bin Alkhatwaab, Allah amuwie radhi, na baada ya kufariki Omari akamuoza binti yake huyo kwa mtoto wa ami yake Jafari bin Abuu Twaalibi hadi alipofariki kisha akaolewa na Auni bin Jafari na kuishi naye hadi binti huyu akafariki.

Na Abdallah bin Jafari Dhii Aljanaahayni bin Abuu Twaalibi alimpa mmoja wa watoto wake jina la Abuu Bakri, na mtoto mwingine akamwita kwa jina la (Muawiya), na Muawiya huyu ambaye ni mtoto wa Abdallah bin Jafari bin Abuu Twaalibi alimwita mmoja wa watoto wake kwa jina la (Yazidu) kwa kuwa alijua kuwa Yazidu alikuwa na mwenendo mzuri, kama ilivyoshuhudiwa hilo kwa Muhammad bin Hanafiya bin Ali bin Abuu Twaalibi.

**Kwa nini tunajitenga nao?**

Ikiwa kujitenga na Maswahaba jambo ambalo Mashia wa sasa wanatutaka tulitenda ili tujikurubishe nao. Jambo hilo limeshazungumzwa, kwa hiyo wale wanaotutaka tulizungumzie, inawapasa watambue kuwa imamu wao wa kwanza ambaye ni Ali bin Abuu twalibi, Allah amuwie radhi, alikuwa amekosea alipowaita watoto wake kwa majina ya Abuu Bakri, Omari na Athumani, pia angekuwa amekosea zaidi pale alipomuozesha binti yake kwa Omari bin Alkhatwaabi, Allah amuwie radhi.

Vilevile Muhammadi bin Hanafiya angekuwa muongo alipotoa ushahidi wa kumtetea Yazidu. Pale Abdallah bin Mutwiiu alipokuja huku akimnadi Ibni Zubeiri na kudai kuwa Yazidu anakunywa pombe, haswali swala tano na anachupa mipaka ya hukumu za Quran. Lakini Muhammadi bin Ali bin Abuu Twaalibu akamwambia (kama ilivyokuja katika kitabu Albidaya Wannihaaya 8:233): Sijamwona akifanya hayo mnayoyasema, nami nilienda kwake na kuishi kwake na kumuona

anatekeleza swala tano, anapupia mambo ya heri, anauliza mambo ya kifiqihi na anapenda sunna…

Ibnu Mutwii na wale aliokuwa nao wakamwambia: Hilo kwake yeye lilikuwa ni kujionesha kwako. Akawajibu: "Kitu gani kilichomfanya aniogope mimi, au kipi kilichombadilisha na kumfanya aoneshe unyenyekevu? Je, mmemuona akinywa pombe? Na kama mmemuona basi nyinyi ni washirika wake katika hilo, na kama hamjamuona basi si halali kwenu kushuhudia msichokijua". Wakasema kwa haki jambo hilo la kunywa pombe, kwetu sisi ni la kweli ijapokua hatujaliona.

Akawaambia: "Allah amekataza jambo hilo kwa wenye kushuhudia shahada mbili pale aliposema, (Ispokuwa wale walishuhudia kwa haki hali ya kuwa wanajua) kwa hiyo jambo lenu halina mpango wowote." Hadi mwisho wa kisa. Ikiwa haya ndiyo anayoyatolea ushahidi mtoto wa Ali bin Abuu Twaalibi juu ya Yazidu. Kikowapi kile Mashia wanachotutaka tukifanye ili tuwe pamoja na baba yake na viumbe bora vyote? Nakusudia Abuu Bakri, Omari, Athumani, Twalha, Zubeiru, Amru bnu Al-Aaswi na Maswahaba wengine waliotuhifadhia kitabu cha Allah na Suna za Mtume wake kisha wakatupatia huu ulimwengu wa Kiislamu tunaouishi sasa hivi.

Kwa hakika thamani ya kile Mashia wanachotutaka tukitoe ili tukurubiane nao ni kubwa mno kiasi ambacho tunapata hasara ya kila kitu wala hatupati chochote. Na mtu mjinga ni yule anayekubali kufanya muamala na mtu anayemtaka afanye naye mkataba wa kujipunja.

Kwa hakika kuelemea na kujitenga kulikojenga itikadi ya Kishia kama alivyolitoa azimio hilo bwana Nnaswir Altwuusiyu, na kutiwa nguvu na Neematullah Almuusawiyu na Alkhuunsaariyu, kwa kweli hali maana nyingine zaidi ya kuibadili dini ya Kiislamu na kuwafanyia uadui wale waliousimamisha Uislamu.

Pia wameongopa pale waliposema kuwa kundi lao ndilo kundi pekee linalotofautiana na makundi mengine katika hali zake.

### Kumeguka kwa Ismailiya kutoka kwa Mashia

Kwa hakika Ismailiya wanafanana na Imamiya kwa kuwa wao nao wanatofautiana na Waislamu wengine katika mambo yale yale wanayotofautiana na Imaamiya ukitoa jambo la kuanisha majina ya Ahlu Beiti wanaowakubali. Maimaamiya wanamtawalisha Musa bin Jafari na wale wote walio wa kizazi chake. Huku Ismailiya wakimtawalisha Ismaili bin Jafari na wale wote walio wa kizazi chake.

Ghuluwu (kuzidisha mno) kulikofanywa na Ismailiya kumhusu Ismaili na waliokuja baada yake, ilihusudiwa na Imaamiya katika zama za utawala wa Dola ya Aswafawiya. Mashia wakatumbukia katika shimo la Ghuluwu, wakiongozwa na Almajlisiyu na wasaidizi wake. Zamani waliokuwa na Ghuluwu ni wachache miongoni mwao, ama kwa sasa wote wana ghuluwu.

Mwazuoni wao mkuu katika elimu ya hadithi ambaye ni Ayatullah Almaqaaniyu katika maelezo yake juu ya maghuluwu wa Kishia wa kale, katika vitabu vyake vyote, ametangaza kila sehemu aliyogusia mada hii hasa katika kitabu chake kikukuu, kuwa kile ambacho watu wa zamani walikiona ni ghuluwu, kwa sasa kimekuwa, kwa Mashia Imaamiya wote ni kitu cha lazima kwa madhehebu yao.

Kwa hiyo, ule ughuluwu uliokuwa kwa Ismailiya kinyume na Mashia Imaamiya kwa sasa unafanywa na Mashia Imaamiya bila ya tofauti yoyote kati yao, ispokuwa tofauti za majina ya watu wanaonyanyuliwa na kutukuzwa hadi kupita sifa za Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake.

Maimaamiya kupitia kauli ya Muhammad Hassan Al-Ashtiyaaniyu wamehalalisha kutomsadikisha Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, hata kama itakuwa ni hadithi sahihi, ikiwa zitakuwa zinahusu mambo ya ghaibu kama vile kuumbwa mbingu na ardhi, na sifa za pepo na moto. Huku wakiwanyanyua na kuwanasibisha na daraja za miungu ya Kiyunani wale Maimamu zao kumi na wawili wanaowaamini.

Kwa hakika kutowezekana kuyakurubisha makundi ya Kiislamu na makundi ya Kishia kunatokana na sababu za Mashia kuwa wao wanahitilafiana na makundi mengine katika misingi ya dini kama anavyokiri na kutangaza Bwana Annaaswiru Altuusiyu. Vilevile, Neematullah Almuusawiy, Baakir na Alkhuunsaariyu wamekiri jambo hilo.

Pia mambo hayo yanakubaliwa na kila Mshia. Ikiwa hizi ndio zama za Annaaswiru Altuusiyu na hizo ndizo zama za Baakir Almajlisiyu, ama leo hii ni hatari na ubaya zaidi. Jambo lisilo na shaka ni kuwa Mashia Imaamiya ndio wasioridhia kukurubiana, ndio maana wanajitahidi kwa kadiri ya uwezo wao kueneza wito wa kukurubiana katika miji yetu ya Kisunni. Huku wakikataa katakata kuueneza wito huo huo katika miji yao ya Kishia, au hata kuona athari za wito huo katika shule na vyuo vya Kishia.

Kwa hiyo wito huo ni wa upande mmoja, kama tulivyotaja mwanzoni mwa makala hii. Kwa hiyo wito huu ni kama nyaya za umeme ambazo

hazigusani chanya na hasi. Matokeo yake, juhudi yeyote katika jambo hili itakuwa ni mchezo usio na tija kama michezo ya kitoto, hadi pale Mashia watakapoacha kumlaani Abuu Bakri na Omari. Pia waache kujitenga na kila asiye Mshia tangu kufariki kwa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, hadi siku ya Kiama.

Vilevile Mashia waache itikadi ya kuwakuza maimamu zao na kuwafikisha daraja za miungu ya Kigiriki, kwa kuwa mambo yote haya, ni kuchupa mipaka ya Uislamu, na kuyapotosha yale yaliyoelekezwa na Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, pamoja na Maswahaba zake wema, akiwemo Ali bin Abuu Twaalibu na watoto zake.

Kama Mashia hawataacha huku kuchupa mipaka dhidi ya Uislamu, itikadi yake na historia yake, wataendelea kutengwe peke yao wakiwa na misingi yao inayotofautiana na misingi ya Waislamu wote. Pia watakuwa wananyanyapaliwa na Waislamu wengine wote.

Kuna jambo la hakika amabalo tumeligusia juu juu mwanzoni mwa makala hii, nalo ni: Ukoministi ulioshika kasi mno huko Iraq na katika chama cha TODA cha Iran, kuliko katika miji mingine ya Kiislamu na hili ni zao la Uishia. Ukoministi katika nchi mbili hizo umejikita zaidi katika kizazi cha Mashia. Kwa kuwa Ukoministi uligundua kuwa Ushia unaamini ngano zisizo sahihi, vitu vya ovyo ovyo na uongo usioingia akilini.

Mashia waliouona Ukoministi ukiwa na wahamasishaji, vitabu kwa lugha mbalimbali, ukiendeshwa kwa njia ya kisayansi na kiuchumi na mambo mengineyo, wakatumbukia ndani yake. Lau wengeijua dini ya Kiislamu kwa asili yake, na wangejifunza kuhusu huo Uislam kwa njia sahihi, sio kwa njia za Kishia, Uislamu ungewakinga wao wasitumbukie katika shimo la Ukoministi.

## Fitina ya Ubaabiya

Ilipotokea fitina ya "BAABU" (mlango) huko Iran kabla ya miaka mia moja iliyopita. Pale Ali Muhammad Shirazi alipodai kuwa yeye ndiye (Baabu) mlango wa Imamu Mahdi anayengojewa. Kisha akajipandisha cheo na kudai kuwa yeye ndiye Imamu Mahdi anayengojewa, akajipatia wafuasi miongoni mwa Mashia wa Irani. Serikali ya Irani ya wakati huo ilimpeleka uhamishoni huyu Ali Muhammad Shirazi huko Azebaijani kwani huko ni sehemu ya Massuni wanaofuata madhehebu ya Hanafiya.

Kwa kuwa watu wa huko ni Massuni, hivyo wana kinga, hawatatumbukia katika ujinga na upotoshaji wake unaotokana na misingi ya Kishia

ambayo inawafanya Mashia wawe wepesi kuhadaika naye na kuupokea wito wake. Serikali ya Irani ya wakati huo haikumpeleka huyu Ali Muhammad Shirazi uhamisho katika mji wa Kishia kwa kuwa tabia za madhehebu ya Kishia ni kukubali ujinga kama huu, na wengi wao wanamfuata mtu huyu. Kwa hiyo kama wangempeleka nchi ya Kishia, wigo wa fitina ungeongezeka.

Vilevile, kama tulivyoona kuwa Ushia umesababisha kuenea kwa madai ya Baabayiina na Bahaaiyiina katika karne iliyopita, pia sasa hivi tunaona kuwa Ushia ndio sababu ya vitendo rejeshi "reactions" vya Wasomi wa Kishia walioamka. Kwani itikadi zao ni za ovyo sana, wala haziendani na watu wenye akili timamu, hawajazikubali wakazikengeuka na kujiunga katika wimbi la Ukoministi. Na Ukoministi nao ukawakaribisha na kuwakumbatia, matokeo yake ukapata wafuasi wengi wa Kishia huko Iraq na Iran kuliko walivyopata katika miji mingine ya Kiislamu wa kissuni.

Haya ndiyo niliyoweza kuyawasilisha, nikifuata mafundisho ya Allah na Mtume wake yanayowataka Waislamu wapeane nasaha wao kwa wao. Namuomba Allah ahifadhi dini na mila yake, pia ahifadhi jengo letu kuu la Kiislamu lisiporomoshwe na wanaotaka kuliporomosha. Pia alihifadhi na vitimbi vya wenye kulifanyia vitimbi hadi siku ya malipo.

Makala haya yameandikwa Qairo – na Muhibbuddini Alkhatwiibu

www.islamic-invitation.com